# العقيدة الصحيحة وما يضادها

# *al-´Aqiydah as-Swahiyhah wa maa yudhwaadduhaa*

[´Aqiydah sahihi na yale yenye kupingana nayo]

*Mwandishi*:

**Imaam ´Abdul-´Aziyz bin ´Abdillaah bin Baaz**

*Tarjama*:

**Abu Bakr Khatwiyb al-Atrush**

00. Dibaji ya kitabu "´al-Aqiydah as-Swahiyhah" .......... 3
01. Kumuamini Allaah .......... 6
02. Kuamini nguzo tano za Uislamu .......... 8
03. Kuamini kuwa Allaah ndiye kaumba viumbe na ndiye anayewaendesha .......... 9
04. Kuamini majina na sifa za Allaah .......... 10
05. Kuwaamini Malaika .......... 14
06. Kuamini Vitabu .......... 15
07. Kuwaamini Mitume .......... 17
08. Kuamini siku ya Mwisho .......... 18
09. Kuamini Qadar .......... 19
10. Mtazamo wa Ahl-us-Sunnah juu ya imani .......... 21
11. Mtazamo wa Ahl-us-Sunnah kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah .......... 22
12. Watu waliopinda kutokamana na ´Aqiydah sahihi .......... 24
13. Utata wa waliokuja nyuma ndio ule ule wa washirikina wa kale .......... 25
14. Radd kwa wakanamungu, Baatwiniyyah na Suufiyyah .......... 27
15. Washirikina wa leo ni waovu zaidi kuliko wale wa kale .......... 29
16. Radd kwa Mu´tazilah, Jahmiyyah na Ashaa´irah .......... 30
17. Uwajibu wa kumuabudu Allaah peke yake .......... 31
18. Hitimisho .......... 35

بسم الله الرحمن الرحيم

## 00. Dibaji ya kitabu "´al-Aqiydah as-Swahiyhah"

Himdi zote anastahiki Allaah. Swalah na salaam zimwendee yule ambaye hakuna Mtume mwingine baada yake, kizazi chake na Maswahabah wake.

Amma ba´d:

Pale ilipokuwa ´Aqiydah sahihi ndio msingi wa Uislamu, ndipo nikaonelea iwe maudhui ya muhadhara. Ni jambo linalojulikana kupitia dalili za Kishari´ah kutoka katika Qur-aan na Sunnah ya kwamba matendo mema yanakubaliwa tu pale yatapokuwa ni yenye kutoka katika ´Aqiydah sahihi. ´Aqiydah ikiwa sio sahihi basi yale matendo na maneno yaliyojengwa juu yake yanabatilika. Amesema (Ta´ala):

وَمَن يَكْفُرْ بِالْإِيمَانِ فَقَدْ حَبِطَ عَمَلُهُ وَهُوَ فِي الْآخِرَةِ مِنَ الْخَاسِرِينَ

**"Na yeyote atakayekufuru imani, basi hakika zimebatilika ‘amali zake - naye Aakhirah atakuwa miongoni mwa waliokhasirika." (05:05)**

وَلَقَدْ أُوحِيَ إِلَيْكَ وَإِلَى الَّذِينَ مِن قَبْلِكَ لَئِنْ أَشْرَكْتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخَاسِرِينَ

**"Hakika umefunuliwa Wahy wewe na kwa wale waliokuwa kabla yako ya kwamba ukifanya shirki bila shaka zitabatilika ‘amali zako na [Aakhirah] utakuwa miongoni mwa waliokhasirika." (39:65)**

Kuna Aayah nyingi zikiwa na maana kama hii. Kitabu cha Allaah na Sunnah za Mtume Wake mwaminifu (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) vimefahamisha kuwa ´Aqiydah sahihi imefupishwa katika kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na Qadar kheri na shari yake. Mambo haya sita ndio misingi ya ´Aqiydah sahihi ambayo imeteremshwa na Kitabu cha Allaah kitukufu na Allaah akamtuma kwayo Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Misingi hii inatoa matawi kila kile ambacho ni wajibu kukiamini katika mambo yaliyofichikana na mambo yote yaliyoelezwa na Allaah na Mtume Wake

(Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Dalili ya misingi hii katika Qur-aan na Sunnah ni nyingi sana. Miongoni mwazo ni maneno ya Allaah (Subhaanah):

لَّيْسَ الْبِرَّ أَن تُوَلُّوا وُجُوهَكُمْ قِبَلَ الْمَشْرِقِ وَالْمَغْرِبِ وَلَٰكِنَّ الْبِرَّ مَنْ آمَنَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَالْمَلَائِكَةِ وَالْكِتَابِ وَالنَّبِيِّينَ

**"Si wema pekee kuelekeza nyuso zenu upande wa mashariki na magharibi, lakini wema khaswa ni anayemuamini Allaah na siku ya Mwisho na Malaika na Kitabu na Manabii." (02:177)**

آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنزِلَ إِلَيْهِ مِن رَّبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ ۚ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لَا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِّن رُّسُلِهِ

**"Mtume ameamini yaliyoteremshwa kwake kutoka kwa Mola wake na waumini [pia wameamini]. Wote wamemwamini Allaah, na Malaika Wake, na Vitabu Vyake, na Mitume Wake; [nao husema]: "Hatutafautishi baina ya yeyote kati ya Mitume Wake." (02:285)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا آمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي نَزَّلَ عَلَىٰ رَسُولِهِ وَالْكِتَابِ الَّذِي أَنزَلَ مِن قَبْلُ ۚ وَمَن يَكْفُرْ بِاللَّهِ وَمَلَائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا بَعِيدًا

**"Enyi mlioamini! Mwaminini Allaah na Mtume Wake na Kitabu alichokiteremsha kwa Mtume Wake na Kitabu alichokiteremsha hapo kabla. Atakayemkufuru Allaah na Malaika Wake na Vitabu Vyake na Mitume Wake na siku ya Mwisho, basi hakika amepotoka upotofu wa mbali." (04:136)**

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Je, hujui kwamba Allaah anajua yale yote yaliyomo mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi." (22:70)**

Kuhusu dalili sahihi zenye kuthibitisha misingi hii ni nyingi sana. Miongoni mwazo ni Hadiyth Swahiyh inayojulikana ambayo Muslim ameipokea katika "as-Swahiyh" yake kupitia kwa kiongozi wa waumini ´Umar bin al-Khattwaab (Radhiya Allaahu ´anh) aliyesimulia kuwa Jibriyl (´alayhis-Salaam) alimuuliza Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuhusu imani ambapo akasema:

*"Imani ni kumuamini Allaah, Malaika Wake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, siku ya Mwisho na kuamini Qadar kheri na shari yake."*[1]

al-Bukhaariy na Muslim wameipokea vilevile kupitia kwa Abu Hurayrah. Misingi hii inatoa matawi kila kile ambacho ni wajibu kwa muislamu kukiamini juu ya Allaah (Subhaanah), mambo ya siku ya Qiyaamah na mambo mengine yaliyofichikana.

[1] Muslim (08), at-Tirmidhiy (2610), an-Nasaa´iy (4990), Abu Daawuud (4695), Ibn Maajah (63) na Ahmad (01/27).

## 01. Kumuamini Allaah

Katika kumuamini Allaah (Subhaanah) ni kuamini kuwa Allah ndiye mungu wa haki anayestahiki ´ibaadah pasi na vyengine vyote. Hilo ni kwa sababu Yeye ndiye muumbaji wa viumbe, mwenye kuwatendea wema, mwenye kusimamia riziki zao na anayejua ya siri yao na yale wanayoyafanya hadharani. Yeye ndiye muweza wa kumlipa mtiifu katika wao na kumuadhibu muasi katika wao. Allaah amewaumba majini na wanaadamu kwa ajili ya ´ibaadah hii na akawamrisha nayo. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ مَا أُرِيدُ مِنْهُم مِّن رِّزْقٍ وَمَا أُرِيدُ أَن يُطْعِمُونِ إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ

**"Sikuumba majini na wanaadamu isipokuwa waniabudu. Sitaki kutoka kwao riziki yoyote na wala sitaki wanilishe. Hakika Allaah ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, madhubuti." (51:56-58)**

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ فِرَاشًا وَالسَّمَاءَ بِنَاءً وَأَنزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجَ بِهِ مِنَ الثَّمَرَاتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ

**"Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Ambae amekuumbeni na wale wa kabla yenu mpate kucha. Ambaye amewafanyieni ardhi kuwa ni tandiko na mbingu kuwa ni paa na akateremsha kutoka mbinguni maji [na] akawatolea kwayo matunda kuwa ni riziki zenu. Basi msimfanyie Allaah washirika na hali ya kuwa nyinyi mnajua." (02:21-22)**

Allaah aliwatuma Mitume na akateremsha vitabu kwa ajili ya kubainisha haki hii na kulingania kwayo na wakati huo huo kutahadharisha yale yenye kupingana nayo. Amesema (Subhaanah):

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)**

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

**"Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimfunulia Wahy ya kwamba: "Hakika hapana mungu wa haki isipokuwa Mimi - basi niabuduni!"" (21:25)**

كِتَابٌ أُحْكِمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِن لَّدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۚ إِنَّنِي لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ

**"Hichi ni Kitabu ambacho Aayah Zake zimetimizwa barabara kisha zikapambanuliwa vizuri kutoka kwa Mwenye hikmah, Mjuzi wa yote; ili msiabudu yeyote isipokuwa Allaah. Hakika mimi ni muonyaji kwenu na mbashiriaji." (11:01-02)**

Uhakika wa ´ibaadah hii ni kumpwekesha Allaah (Subhaanah) katika yale yote ambayo waja wanaabudu kwayo katika du´aa, khofu, kutaraji, swalah, swawm, kuchinja, kuweka nadhiri na aina nyenginezo za ´ibaadah. Mtu anatakiwa kufanya yote hayo kwa njia ya kumnyenyekea, kuwa na shauku, kumwogopa na wakati huo huo kuwa na mapenzi kamilifu Kwake (Subaanah) na kumdhalilikia kwa sababu ya ukubwa Wake. Sehemu kubwa ya Qur-aan tukufu imeteremka juu ya msingi huu mkubwa. Amesema (Subhaanah):

فَاعْبُدِ اللَّهَ مُخْلِصًا لَّهُ الدِّينَ أَلَا لِلَّهِ الدِّينُ الْخَالِصُ

**"Mwabudu Allaah hali ya kumtakasia Yeye dini! Tanabahi, ni ya Allaah pekee dini iliyotakasika." (39:02-03)**

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ

**"Mola wako ameamrisha, kwamba asiabudiwe yeyote isipokuwa Yeye pekee." (17:23)**

فَادْعُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ

**"Basi mwombeni Allaah hali ya kumtakasia Yeye dini japokuwa wanachukia makafiri." (40:14)**

al-Bukhaariy na Muslim wamepokea kutoka kwa Mu´aadh (Radhiya Allaahu ´anh) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

*"Haki ya Allaah juu ya waja wamuabudu Yeye na wala wasimshirikishe na chochote."*[2]

[2] al-Bukhaariy (2701), Muslim (30), at-Tirmidhiy (2643), Ibn Maajah (4296) na Ahmad (05/238).

## 02. Kuamini nguzo tano za Uislamu

Katika kumuamini Allaah kunaingia vilevile kuamini yale yote aliyoyawajibisha na kuyafaradhisha kwa waja Wake katika nguzo za Uislamu tano za dhahiri ambazo ni kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah, kusimamisha swalah, kutoa zakaah, kufunga Ramadhaan, kuhiji Nyumba ya Allaah tukufu kwa mwenye kuweza kuiendea na mambo mengine ambayo yameletwa na Shari´ah takasifu.

Nguzo muhimu na kubwa zaidi ni kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah na kwamba Muhammad ni Mtume wa Allaah. Kushuhudia ya kwamba hapana mungu wa haki isipokuwa Allaah kunapelekea kumtakasia ´ibaadah Allaah pekee na kumkanushia nayo asiyekuwa Yeye. Hii ndio maana ya "Laa ilaaha illa Allaah". Maana yake ni hakuna muabudiwa wa haki isipokuwa Allaah. Kila chenye kuabudiwa katika watu, Malaika, jini na vyenginevyo ni vyenye kuabudiwa kwa batili. Muabudiwa wa haki ni Allaah peke yake. Amesema (Subhaanah):

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِن دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ

**"Hivyo ni kwa kuwa Allaah ndiye wa haki na kwamba vile [makafiri] wanavyoomba badala Yake ndiyo batili." (22:62)**

Tumetangulia kusema kuwa Allaah (Subhaanah) amewaumba majini na watu kwa ajili ya msingi wa misingi huu na akawaamrisha nao. Kadhalika amewatuma Mitume na akateremsha vitabu kwa lengo hilo. Hivyo basi zingatia hilo vizuri ili ipate kukubainikia ule ujinga mkubwa waliyotumbukia kwao waislamu juu ya msingi wa misingi huu na matokeo yake wakamuabudu Allaah pamoja na wengine na vilevile wakawatekelezea wengine haki ambayo ni maalum Kwake. Allaah ndiye Mwenye kutakwa msaada.

## 03. Kuamini kuwa Allaah ndiye kaumba viumbe na ndiye anayewaendesha

Katika kumuamini Allaah (Subhaanah) kunaingia vilevile kuamini kuwa Allaah ndiye kaumba ulimwengu na ndiye Mwenye kuyaendesha mambo yao kwa ujuzi na uwezo Wake kama alivyotaka (Subhaanah). Vilevile kuamini kuwa Yeye ndiye mfalme wa dunia na Aakhirah na Mola wa walimwengu wote. Hakuna muumba mwingine asiyekuwa Yeye na hakuna Mola asiyekuwa Yeye. Amewatuma Mitume na akateremsha vitabu ili kuwatengeneza waja na kuwaita katika yatayowafanya kuokoka duniani na Aakhirah. Inatakiwa vilevile kuamini kuwa Yeye (Subhaanah) hana mshirika katika yote hayo. Amesema (Ta´ala):

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

**"Allaah ni Muumbaji wa kila kitu Naye juu ya kila kitu ni mdhamini anayetegemewa." (39:62)**

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ
مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi. Anafunika usiku kwa mchana, unaufuatia upesi upesi na jua na mwezi na nyota vyote vimetiishwa kwa amri Yake. Tanabahi! Ni Vyake Pekee uumbaji na amri. Amebarikika Allaah, Mola wa walimwengu." (07:54)**

## 04. Kuamini majina na sifa za Allaah

Katika kumuamini Allaah inatakiwa vilevile kuamini majina Yake mazuri na sifa Zake kuu zilizothibiti katika Qur-aan na Sunnah. Mtu anatakiwa afanye hivo bila ya kupotosha, kukanusha, kuziwekea namna na kuzifananisha. Bali ni wajibu kuyapitisha kama yalivyokuja bila ya kuyafanyia namna pamoja na kuamini ile maana tukufu iliyofahamishwa nayo ambayo ni sifa ya Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala). Ni wajibu kumsifu nazo kwa njia inayolingana Naye. Inatakiwa kufanya hivo pasi na kumshabihisha na viumbe Vyake kwenye chochote katika hayo. Amesema (Ta´ala):

لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ ۖ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ

**"Hakuna chochote kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona." (42:11)**

فَلَا تَضْرِبُوا لِلَّهِ الْأَمْثَالَ ۚ إِنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ وَأَنتُمْ لَا تَعْلَمُونَ

**"Basi msimpigie Allaah mifano. Hakika Allaah anajua nanyi hamjui." (16:74)**

Hii ndio ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kuanzia kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wale waliowafuata kwa wema. Nayo ndio iliyonukuliwa na Imaam Abul-Hasan al-Ash´ariy (Rahimahu Allaah) katika kitabu "al-Maqaalaat ´an Aswhaab-il-Hadiyth wa Ahl-is-Sunnah". Imenukuliwa vilevile na wanachuoni na watu wa imani wengine.

al-Awzaa´iy (Rahimahu Allaah) amesema: "az-Zuhriy na Mak-huul waliulizwa kuhusu Aayah za sifa za Allaah ambapo wakasema:

"Zipitishe kama zilivyokuja."

al-Waliyd bin Muslim (Rahimahu Allaah) amesema: "Maalik, al-Awzaa´iy, al-Layth bin Sa´d na Suufyaan ath-Thawriy waliulizwa kuhusu Aayah zinazozungumzia sifa za Allaah ambapo wote wakasema:

"Zipitishe kama zilivyokuja pasi na kuzifanyia namna."

al-Awzaa´iy (Rahimahu Allaah) amesema:

"Tulikuwa tukisema, na Taabi´uun wamejaa, ya kwamba Allaah (Subhaanah) amelingana juu ya ´Arshi" na tukiamini vilevile sifa zilizothibiti katika Sunnah.""

Pindi Rabiy´ah bin Abiy ´Abdir-Rahmaan, ambaye ni mwalimu wa Maalik (Rahimahumaa Allaah), alipoulizwa kuhusu kulingana alisema:

"Kulingana kunajulikana. Namna haitambuliki. Ujumbe ni wenye kutoka kwa Allaah. Ni juu ya Mtume kufikisha kuliko wazi. Ni juu yetu kusadikisha."

Wakati Imaam Maalik (Rahimahu Allaah) alipoulizwa kuhusu hilo alisema:

"Kulingana kunajulikana. Namna haijulikani. Kuamini hilo ni wajibu. Kuulizia hilo ni Bid´ah." Baada ya hapo alimwambia yule muulizaji:

"Mimi sikuoni wewe isipokuwa ni mtu muovu."

Halafu akaamrisha atolewe nje.

Maana kama hii imepokelewa kutoka kwa mama wa waumini Umm Salamah (Radhiya Allaahu ´anhaa).

Imaam Abu ´Abdir-Rahmaan bin al-Mubaarak (Rahimahu Allaah) amesema:

"Tunamtambua Mola wetu (Subhaanah) ya kwamba yuko juu ya mbingu, juu ya ´Arshi na ametengana na viumbe Wake."

Maneno ya maimamu kuhusiana na mada hii ni mengi sana. Hatuwezi kuyanukuu yote katika muhadhara huu. Anayetaka kusoma mengi katika hayo basi arejee yale yaliyoandikwa na wanachuoni wa Sunnah katika mlango huu. Mfano wa kitabu "as-Sunnah" cha ´Abdullaah bin Imaam Ahmad, "Kitaab-ut-Tawhiyd" cha Imaam mtukufu Muhammad bin Khuzaymah, "as-Sunnah" cha Abul-Qaasim al-Laalakaa´iy at-Twabariy, "as-Sunah" cha Abu Bakr bin Abiy ´Aaswim, "al-Hamawiyyah" cha Shaykh-ul-Islaam Ibn Taymiyyah ambacho ni jibu kubwa na lililo na faida nyingi. Ndani yake ameweka wazi (Rahimahu Allaah) ´Aqiydah ya Ahl-us-Sunnah na humo vilevile amenukuu maneno yao mengi na dalili za Kishari´ah na za kiakili juu ya usahihi wa yale waliyosema Ahl-us-Sunnah na ubatilifu wa yale waliyosema wapinzani wao. Vilevile inahusiana na kitabu chake kwa jina "at-Tadmuriyyah" ambapo ndani yake amekipanua na amebainisha ´Aqiydah ya

Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah kwa kutumia dalili za kinukuu na za kiakili na wakati huo huo kuwaraddi wenye kwenda kinyume. Ameidhihirisha haki na kuiponda batili. Hilo linatambulika na kila mwanachuoni mwenye kuvisoma kwa nia njema hali ya kuwa ni mwenye kukusudia kuijua haki. Kila yule mwenye kwenda kinyume na Ahl-us-Sunnah katika yale wanayoitakidi katika mlango wa majina na sifa za Allaah ni lazima atumbukie katika kuzikhalifu dalili za kinukuu na za kiakili pamoja vilevile na kujigonga kwa wazi katika yale yote atayoyathibitisha na kuyakanusha.

Kuhusu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanamthibitishia Allaah (Subhaanahu wa Ta´ala) yale aliyojithibitishia Mwenyewe katika Qur-aan au yale aliyothibitishiwa na Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) katika Sunnah Swahiyh. Uthibitishaji huu unafanyika bila ya ufananishaji na vilevile anatakaswa (Subhaanah) kushabihiana na viumbe Wake ambapo inakuwa ni utakasaji ulio mbali na ukanushaji. Kwa ajili hiyo wakafuzu kwa usalama kutokamana na kujigonga na wakazifanyia kazi dalili zote. Huu ndio mwenendo wa Allaah. Ambaye anashikamana na haki aliyomtuma nayo Mtume Wake, akatumia juhudi zake katika hilo na akamtakasia nia Allaah katika kuitafuta humuwafikisha katika haki na humfanya hoja yake ikashinda. Amesema (Ta´ala):

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ

**"Bali Tunavurumisha haki dhidi ya batili inaivunja; tahamaki [batili] inatoweka." (21:18)**

وَلَا يَأْتُونَكَ بِمَثَلٍ إِلَّا جِئْنَاكَ بِالْحَقِّ وَأَحْسَنَ تَفْسِيرًا

**"Wala hawakujii kwa mfano wowote isipokuwa Tunakuletea haki na tafsiri nzuri kabisa." (25:33)**

Haafidhw Ibn Kathiyr (Rahimahu Allaah) amesema maneno mazuri katika Tafsiyr yake inayojulikana kuhusiana na maneno ya Allaah:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi." (07:54)**

Niyatanukuu hapa kutokana na ukubwa wa faida yake. Amesema (Rahimahu Allaah) yafuatayo:

"Watu hapa wana maoni mengi sana. Hapa sio mahala pa kuyajadili. Mahala hapa tutasimulia madhehebu ya as-Salaf as-Swaalih; Maalik, al-Awzaa´iy, ath-Thawriy, al-Layth bin Sa´d, ash-Shaafi´iy, Ahmad, Ishaaq bin Raahuuyah na maimamu wengine wa waislamu wa kale na waliokuja baadae. Nayo ni kuyapitisha kama yalivyokuja pasi na kuyafanyia namna, kuyashabihisha, wala kuyakanusha. Inavyoonekana kitu kinachokuja kwa haraka kwenye akili ya wale wenye kuzifananisha sifa za Allaah na za viumbe Wake ni kumkanushia nayo Allaah. Hakika Allaah hafanani na chochote katika viumbe Wake. Hakuna kitu kinachofanana Naye - Naye ni Mwenye kusikia, Mwenye kuona. Mambo yalivyo ni kama walivyosema maimamu, ambapo mmoja wao ni Na´iym bin Hammaad al-Khuzaa´iy, ambaye ni mwalimu wa al-Bukhaariy, aliyesema:

"Mwenye kumshabihisha Allaah na viumbe Wake anakufuru. Anayemkanushia Allaah yale aliyojisifia Mwenyewe anakufuru. Hakuna katika yale Allaah aliyojithibitishia Mwenyewe na Mtume Wake ushabihishaji."

Atayemthibitishia Allaah (Ta´ala) yale yaliyothibiti katika Aayah zilizo wazi na maelezo Swahiyh kwa njia inayolingana na utukufu wa Allaah na wakati huo huo akamkanushia Allaah (Ta´ala) kasoro, basi amefuata njia ya uongofu."

## 05. Kuwaamini Malaika

Kuhusu kuwaamini Malaika kunajumuisha kuwaamini kwa jumla na kwa upambanuzi. Muislamu anatakiwa kuamini kuwa Allaah ana Malaika aliowaumba ili wamtii na ambao amewasifu kuwa ni waja watukufu ambao hawamtangulii kwa neno na kwa maamrisho Yake ni wenye kuyatendea kazi. Amesema (Ta´ala):

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ ارْتَضَىٰ وَهُم مِّنْ خَشْيَتِهِ مُشْفِقُونَ

**"Anajua yale yaliyoko mbele yao na yale yaliyoko nyuma yao na wala hawamuombei uombezi isipokuwa yule ambaye Amemridhia. Nao kutokana na kumkhofu ni wenye kutahadhari." (21:28)**

Wana kazi mbalimbali. Katika wao kuko ambao kazi yao ni kuibeba ´Arshi, walinzi wa Pepo na Moto na wengine kazi yao ni kuyadhibiti matendo ya waja. Vilevile tunatakiwa kuwaamini kwa njia ya upambanuzi wale ambao wametajwa na Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Katika hao ni kama Jibriyl, Mikaaiyl, Maalik, ambaye ni mlinzi wa Moto, na Israafiyl, ambaye kazi yake ni kupuliza baragumu. Wametajwa katika Hadiyth ambazo ni Swahiyh. Imethibiti katika "as-Swahiyh" kupitia kwa ´Aaishah (Radhiya Allaahu ´anhaa) ya kwamba Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

*"Malaika wameumbwa kutokana na nuru, majini wameumbwa kutokana na mwako wa moto na Aadam ameumbwa kutokana na kile mlichoelezewa."*[3]

Ameipokea Muslim katika "as-Swahiyh" yake.

[3] Muslim (2996) na Ahmad (06/153).

## 06. Kuamini Vitabu

Vivyo hivyo inahusiana na kuamini Vitabu. Ni wajibu kuamini kwa jumla ya kwamba Allaah (Subhaanah) amewateremshia Vitabu Manabii na Mitume Wake kwa ajili ya kubainisha haki na kulingania katika dini Yake. Amesema (Ta´ala):

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ

**"Hakika Tuliwatuma Mitume Wetu kwa hoja bayana na Tukateremsha pamoja nao Kitabu na mizani ili watu wasimamie kwa uadilifu." (57:25)**

كَانَ النَّاسُ أُمَّةً وَاحِدَةً فَبَعَثَ اللَّهُ النَّبِيِّينَ مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ وَأَنزَلَ مَعَهُمُ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِيَحْكُمَ بَيْنَ النَّاسِ فِيمَا اخْتَلَفُوا فِيهِ

**"Watu walikuwa ummah mmoja kisha Allaah akawatuma Mitume wabashiriaji na waonyaji na akateremsha pamoja nao Kitabu kwa haki ili kihukumu baina ya watu katika waliyokhitilafiana kwayo." (02:213)**

Vilevile inatupasa kuamini kwa njia ya upambanuzi vile ambavyo Allaah amevitaja. Mfano wa hivyo ni Tawraat, Injiyl, az-Zabuur na Qur-aan. Qur-aan ndio bora zaidi, ndio cha mwisho, ndio yenye kuvihukumu na ndio yenye kuvisadikisha. Ni wajibu kwa watu wote kuiamini, kuifuata na kuhukumu kwacho pamoja na zile Sunnah zilizosihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa kuwa Allaah (Subhaanah) amemtuma Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) hali ya kuwa ni Mtume kwa majini na wanaadamu na vilevile akamteremshia Qur-aan hii ili aweze kuhukumu kwayo na akaifanya kuwa ni shifaa kwa yale yaliyomo kifuani na yenye kubainisha kila kitu na ni mwongozo na huruma kwa waumini. Amesema (Ta´ala):

وَهَٰذَا كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

**"Kitabu hiki Tumekiteremsha kilichobarikiwa, basi kifuateni na cheni mpate kurehemewa." (06:155)**

وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِّكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَىٰ لِلْمُسْلِمِينَ

**"Tumekuteremshia Kitabu chenye kubainisha kila kitu na ni mwongozo na Rahmah na bishara kwa waislamu." (16:89)**

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ ۖ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ الْأُمِّيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَاتَّبِعُوهُ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

**"Sema: "Hakika mimi ni Mtume wa Allaah kwenu nyinyi nyote; Yeye ambaye pekee anao ufalme wa mbingu na ardhi. Hapana mungu wa haki isipokuwa Yeye, anayehuisha na kufisha. Basi mwaminini Allaah na Mtume Wake, Nabii asiyejua kuandika wala kusoma, ambaye anamwamini Allaah na maneno Yake - mfuateni ili mpate kuongoka." (07:158)**

Kuna Aayah nyingi zilizo na maana kama hii.

## 07. Kuwaamini Mitume

Hali kadhalika inahusiana na Mitume. Ni wajibu kuwaamini kwa jumla na kwa upambanuzi. Tunatakiwa kuamini kuwa Allaah (Subhaanah) amewatumia waja Wake Mitume wenye kutoa bishara njema na maonyo na wanaolingania katika haki. Atayewaitikia basi huyo amefuzu kwa furaha na atayewakhalifu huyo amekula khasara na majuto. Mtume wa mwisho na ambaye ni bora ni Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Allaah (Subhaanah) amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)**

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ الرُّسُلِ

**"Mitume ambao ni wabashiriaji na waonyaji ili pasikuweko kutoka kwa watu hoja yoyote juu ya Allaah baada ya Mitume [hao kuletwa]." (04:165)**

مَّا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِّن رِّجَالِكُمْ وَلَٰكِن رَّسُولَ اللَّهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ

**"Muhammad hakuwa ni baba wa yeyote miongoni mwa wanaume wenu, lakini ni Mtume wa Allaah na ni mwisho wa Manabii." (33:40)**

Wale waliotajwa na Allaah na wamethibiti kutajwa na Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), basi tunatakiwa kumuamini kwa njia ya upambanuzi na kwa dhati zao kama mfano wa Nuuh, Huud, Swaalih, Ibraahiym na wengineo (´alayhim-us-Swalaatu was-Salaam).

## 08. Kuamini siku ya Mwisho

Kuhusu kuamini siku ya Mwisho kunaingia kuamini yale yote yatayotokea baada ya kufa aliyoelezea Allaah na Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Mfano wa mambo hayo ni kama fitina ya adhabu ya kaburi na neema zake. Vilevile na yale yatayokuwa siku ya Qiyaamah katika hali nzito, njia, mizani, hesabu, malipo, kutawanya madaftari kati ya watu; kuko ambao watapokea madaftari yao kwa mkono wa kulia na wengine watapokea madaftari yao kwa mkono wa kushoto au nyuma ya migongo yao. Kunaingia vilevile kuamini hodhi iliyothibiti ya Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Pepo na Moto, waumini kumuona Mola Wao (Subhaanah), kwamba atawazungumzisha na mengineyo yaliyotajwa katika Qur-aan tukufu na Sunnah Swahiyh kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Ni wajibu kuyaamini na kuyasadikisha yote hayo kwa njia aliyoibainisha Allaah na Mtume Wake.

## 09. Kuamini Qadar

Kuhusu kuamini Qadar ndani yake kunaingia kuamini mambo mane:

**La kwanza:** Allaah (Subhaanah) ameyajua yaliyokuwepo, yatayokuwepo, amezijua hali za waja, amezijua riziki zao, muda wao wa kueshi, matendo yao na mengine katika mambo yao. Hakuna chochote katika hayo kinachofichikana Kwake (Subhaanahu wa Ta´ala). Amesema (Subhaanah):

أَنَّ اللَّهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

**"Hakika Allaah juu ya kila kitu ni mjuzi." (02:231)**

لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

**"... ili mpate kujua kwamba Allaah juu ya kila kitu ni muweza na kwamba Allaah amekwishakizunguka kila kitu kwa ujuzi." (65:12)**

**La pili:** Ameyaandika (Subhaanah) yale yote aliyoyakadiria na kuyapanga. Amesema (Subhaanah):

قَدْ عَلِمْنَا مَا تَنقُصُ الْأَرْضُ مِنْهُمْ ۖ وَعِندَنَا كِتَابٌ حَفِيظٌ

**"Hakika Sisi tunajua kinachopunguzwa na ardhi kutokana nao [miili yao iliyokufa] na tunacho Kitabu kinachohifadhi." (50:04)**

وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ

**"Kila kitu Tumekirekodi barabara katika kitabu kinachobainisha." (36:12)**

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَٰلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ

**"Je, hujui kwamba Allaah anajua yale yote yaliyomo mbinguni na ardhini? Hakika hayo yamo katika Kitabu. Hakika hayo kwa Allaah ni mepesi." (22:70)**

**La tatu:** Kuamini matakwa Yake yenye kutendeka. Anayoyataka, hutokea, na asiyoyataka, hayatokei. Amesema (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ

**"Hakika Allaah anafanya atakavyo." (22:18)**

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَن يَقُولَ لَهُ كُن فَيَكُونُ

**"Hakika amri Yake anapotaka chochote kile hukiambia: "Kuwa!" - nacho huwa." (36:82)**

وَمَا تَشَاءُونَ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا

**"Hamtotaka chochote isipokuwa atake Allaah; hakika Allaah daima ni mjuzi, Mwenye hikmah." (76:30)**

**La nne:** Kuumba Kwake (Subhaanah) vile vyote vilivyopo. Hakuna muumbaji mwingine wala Mola asiyekuwa Yeye. Amesema (Subhaanah):

اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ ۖ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ

**"Allaah ni Muumbaji wa kila kitu Naye juu ya kila kitu ni mdhamini anayetegemewa." (39:62)**

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اذْكُرُوا نِعْمَتَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ ۚ هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللَّهِ يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۚ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۖ فَأَنَّىٰ تُؤْفَكُونَ

**"Enyi watu! Kumbukeni neema za Allaah juu yenu. Je, kuna muumbaji mwingine badala ya Allaah anayekuruzukuni kutoka mbinguni na kwenye ardhi? Hapana mungu wa haki isipokuwa Yeye, basi mbona mnageuzwa?" (35:03)**

Kuamini Qadar kunajumuisha kuamini mambo haya mane kwa mujibu wa Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah. Hivyo ni tofauti na baadhi ya Ahl-ul-Bid´ah waliopinga baadhi ya mambo hayo.

## 10. Mtazamo wa Ahl-us-Sunnah juu ya imani

Katika kumuamini Allaah kunaingia vilevile kuitakidi kuwa imani ni maneno na matendo. Imani inazidi kwa utiifu na inapungua kwa maasi na kwamba haijuzu kumkufurisha muislamu yeyote kwa dhambi aliyoifanya ilio chini ya shirki na kufuru. Mfano wa dhambi hizo ni kama uzinzi, kuiba, kula ribaa, kunywa pombe, kuwaasi wazazi na dhambi nyenginezo kubwa midhali hajahalalisha hayo. Amesema (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَٰلِكَ لِمَن يَشَاءُ

**"Hakika Allaah hasamehi kushirikishwa na anasamehe yaliyo chini ya hayo kwa amtakae." (04:48)**

Vilevile kutokana na yale yaliyothibiti katika Hadiyth zilizopokelewa kwa mapokezi mengi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) ya kwamba Allaah atawatoa Motoni wale ambao moyoni mwao walikuwa na imani sawa na uzito wa mbegu ya haradali.

## 11. Mtazamo wa Ahl-us-Sunnah kwa Maswahabah wa Mtume wa Allaah

Katika kumuamini Allaah kunaingia vilevile kupenda na kuchukia kwa ajili ya Allaah na kujenga urafiki na uadui kwa ajili ya Allaah. Muumini anatakiwa kuwapenda waumini na kujenga nao urafiki na anatakiwa vilevile kuwachukia makafiri na kujenga kwao uadui. Waumini wanaochukua nafasi ya mbele katika Ummah huu ni Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Kwa hiyo Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wanawapenda na kujenga nao urafiki na vilevile wanaonelea kuwa wao ndio watu bora baada ya Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

*"Karne bora ni karne yangu. Kisha wataofuatia. Kisha wataofuatia."*[4]

Kuna maafikiano juu ya usahihi wake.

Wanaitakidi kuwa mbora wao ni Abu Bakr asw-Swiddiyq, halafu ´Umar al-Faaruq, halafu ´Uthmaan Dhun-Nuurayn kisha ´Aliy al-Murtadhwaa (Radhiya Allaahu ´anhum).

Baada yao wanaofuata ni wale Maswahabah kumi wengine waliobakia halafu Maswahabah wengine waliobaki (Radhiya Allaahu ´anhum).

Wananyamazia yale yote yaliyopitika kati ya Maswahabah na wakati huo huo wanaonelea kuwa katika hayo walikuwa ni wenye kufanya Ijtihaad. Aliyepatia basi ana ujira mara mbili na aliyekosea ana ujira mara moja.

Vilevile wanawapenda watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) waliomuamini na wanajenga urafiki nao na wakeze Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), ambao ndio mama wa waumini, na wanawatakia radhi wote kwa pamoja. Ahl-us-Sunnah ni wenye kujitenga mbali kabisa na mfumo wa Raafidhwah ambao wanawachukia Maswahabah wa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na kuwatukana na sambamba na hilo wanapetuka kwa watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na wanawanyanyua zaidi ya nafasi zao walizopewa na Allaah. Ahl-us-Sunnah vilevile wanajitenga mbali kabisa na

[4] al-Bukhaariy (2509), Muslim (2533), at-Tirmidhiy (3859), Ibn Maajah (2362) na Ahmad (01/434).

mfumo wa Nawaaswib ambao wanawaudhi watu wa familia ya Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) aidha kwa maneno au vitendo.

Yale yote tuliyoyataja katika maneno haya machache yanaingia katika ´Aqiydah sahihi ambayo Allaah amemtuma nayo Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Hiyo ndio ´Aqiydah ya Firqat-un-Naajiyah[5], Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah, ambao Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema juu yao:

*"Hakitoacha kikundi katika Ummah wangu kuwa juu ya haki hali ya kuwa ni chenye kunusuriwa. Hakitodhurika na wale wenye kuwakosesha nusura mpaka ifike amri ya Allaah (Subhaanah)."*[6]

*"Mayahudi wamefarikiana mapote sabini na moja na wakristo wamefarikiana mapote sabini na mbili. Ummah huu utakuja kufarikiana mapote sabini na tatu. Yote yataingia Motoni isipokuwa moja tu." Maswahabah wakauliza: "Ni lipi hilo, ee Mtume wa Allaah?" Akasema: "Ni wale wataokuwa juu ya yale niliyomo mimi na Maswahabah wangu.""*[7]

Nayo si mengine ni ile ´Aqiydah ambayo ni wajibu kuiamini, kuwa na msimamo juu yake na kutahadhari na yale yanayoenda kinyume nayo.

---

[5] Kundi lililookoka.

[6] Muslim (1920), at-Tirmidhiy (2229), Abu Daawuud (4252), Ibn Maajah (3952) na Ahmad (05/279).

[7] Ibn Maajah (3992).

## 12. Watu waliopinda kutokamana na ´Aqiydah sahihi

Kuna sampuli mbalimbali za watu waliopinda kutokamana na ´Aqiydah hii na wakafuata yale yenye kupingana nayo. Miongoni mwao kuko wenye kuabudu masanamu, mizimu, Malaika, mawalii, majini, miti, mawe na vinginevyo. Watu hawa hawakuitikia ulinganizi wa Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam). Bali wameenda kinyume nao na wakakaidi. Hivyo ndivyo Quraysh na makabila mengine ya kiarabu walivyomfanyia Mtume wetu Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam). Watu hawa walikuwa wakiwaomba waungu wao wawatatulie haja zao, wawaponye maradhi na wawanusuru dhidi ya maadui wao. Vilevile walikuwa wakiwachinjia na wakiwawekea nadhiri. Pindi Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alipowakemea kufanya hivo na badala yake akawaamrisha wamtakasie ´ibaadah Allaah peke yake, walishangzwa na hilo na wakamkemea hali ya kusema:

أَجَعَلَ الْآلِهَةَ إِلَٰهًا وَاحِدًا ۖ إِنَّ هَٰذَا لَشَيْءٌ عُجَابٌ

**"Amewafanya waungu wote hawa kuwa ni mungu Mmoja? Hakika hili ni jambo la ajabu mno!" (38:05)**

Hata hivyo hakuacha (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kuwalingania katika dini ya Allaah na wakati huo huo akiwatahadharisha shirki na akiwawekea wazi uhakika wa yale anayowalingania kwayo mpaka Allaah akawaongoza katika wao aliwaongoza. Baada ya hapo wakaingia katika dini ya Allaah makundi kwa makundi. Hatimae dini ya Allaah ikadhihiri juu ya dini zengine baada ya ulinganizi wenye kuendelea na mapambano marefu ya Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam), Maswahabah (Radhiya Allaahu ´anhum) na wale waliowafuata kwa wema. Baada ya hapo mambo yakabadilika na ujinga ukawa mwingi kwa watu mpaka wengi wakarudi katika dini ya kipindi cha washirikina kwa kupetuka mpaka kwa Mitume, mawalii, kuwaomba du´aa, kuwataka uokozi na aina nyenginezo za shirki. Hawakuelewa maana ya "Laa ilaaha illa Allaah" kama walivyoelewa maana yake makafiri wa kiarabu. Allaah ndiye mwenye kutakwa msaada. Mpaka hii leo watu hawajaacha kuwa na shirki kama hii kutokana na sababu ya kuwa na ujinga mwingi na kuwa mbali na zama za utume.

## 13. Utata wa waliokuja nyuma ndio ule ule wa washirikina wa kale

Utata wa watu hawa waliokuja nyuma ndio utata ule ule wa wale wa kale. Utata wenyewe wanasema kuwa wawaombao ni waombezi wao mbele ya Allaah na kwamba hawawaombi isipokuwa ili wawakurubishe kwa Allaah. Allaah amebatilisha utata huu na kubainisha kuwa atayemuabudu asiyekuwa Yeye - yeyote awae - amemshirikisha na amekufuru. Hivyo ndivyo alivyosema (Ta´ala). Allaah (Subhaanah) amewaraddi kwa kusema:

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَلَا يَنفَعُهُمْ وَيَقُولُونَ هَٰؤُلَاءِ شُفَعَاؤُنَا عِندَ اللَّهِ

**"Wanaabudu asiyekuwa Allaah ambao hawawezi kuwadhuru na wala hawawezi kuwanufaisha na wanasema: "Hawa ni waombezi wetu mbele ya Allaah." (39:03)**

Allaah (Subhaanah) akawaraddi kwa kusema:

إِنَّ اللَّهَ يَحْكُمُ بَيْنَهُمْ فِي مَا هُمْ فِيهِ يَخْتَلِفُونَ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ

**"Hakika Allaah atahukumu baina yao katika yale waliyokhitilafiana nayo. Hakika Allaah hamwongoi aliye muongo kafiri." (39:03)**

Katika Aayah hii amebainisha (Subhaanah) kuwa kumuabudu asiyekuwa Yeye katika Mitume, mawalii na wengineo ya kwamba ni shirki kubwa. Haijalishi kitu hata kama mwenye kufanya hivo atayaita kwa majina mengine. Amesema (Ta´ala):

وَالَّذِينَ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ أَوْلِيَاءَ مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

**"Wale waliojichukulia badala Yake walinzi [wakisema]: "Hatuwaabudu isipokuwa ili watukurubishe kwa Allaah ukaribio."" (39:03)**

Allaah akawaraddi kwa kusema (Subhaanah):

إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ كَاذِبٌ كَفَّارٌ

**"Hakika Allaah hamwongoi aliye muongo kafiri." (39:03)**

Amebainisha (Subhaanah) ya kwamba kule kuwaabudu kwao wengine kwa kuwaomba, kuwa na khofu kwao, kuwatarajia na mengineyo ni kumkufuru (Subhaanah) na akawakadhibisha vilevile ya kwamba waungu wao wanawakurubisha Kwake.

## 14. Radd kwa wakanamungu, Baatwiniyyah na Suufiyyah

Miongoni mwa I´tiqaad za kikafiri zinazopingana na ´Aqiydah sahihi na yale waliyokuja nayo Mitume (Swalla Allaahu ´alayhim wa sallam) ni pamoja na yale wanayoitakidi wakanamungu hii leo katika wafuasi wa Marx, Lenin na walinganizi wengineo wa ukanamungu na ukafiri. Ni mamoja wakayaita hayo ujamaa, ukomunisti, Ba´thiyyah na mengineyo. Hakika miongoni mwa misingi ya wakanamungu hawa ni pamoja vilevile na kuonelea kuwa hakuna mungu na kwamba kuna maisha haya tu ya kidunia. Miongoni mwa misingi yao vilevile ni pamoja na kukanusha kufufuliwa, Pepo na Moto na wanakana dini zote. Atayajua hayo kiyakini yule atayesoma vitabu vyao na yale wanayoamini. Ni jambo lisilokuwa na shaka ya kwamba I´tiqaad hii inapingana na dini zote za kimbingu. Hakika wenye nayo yatawapelekea katika matokeo mabaya duniani na Aakhirah.

Miongoni mwa I´tiqaad batili pia ni pamoja vilevile na yale wanayoitakidi baadhi ya Baatwiniyyah na Suufiyyah ya kwamba baadhi ya wale wanaowaita "mawalii" wanashirikiana na Allaah katika kuyaendesha mambo na wanashiriki pia katika kuendesha kazi za ulimwengu na wanawaita waungu wao "Aqtwaab", "Awtaad", "Aghwaath" na majina mengine waliyoyazusha wao wenyewe. Hii ni shirki mbaya kabisa katika uola wa Allaah. Shirki hii ni mbaya zaidi kuliko shirki ya kipindi cha washirikia wa kiarabu. Washirikina wa kiarabu hawakushirikisha katika uola wa Allaah. Walishirikisha katika ´ibaadah. Isitoshe walikuwa wakishirikisha katika kipindi cha raha. Kuhusiana na kipindi cha shida walikuwa wakimtakasia ´ibaadah Allaah pekee. Allaah (Subhaanah) amesema:

فَإِذَا رَكِبُوا فِي الْفُلْكِ دَعَوُا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ فَلَمَّا نَجَّاهُمْ إِلَى الْبَرِّ إِذَا هُمْ يُشْرِكُونَ

**"Wanapopanda merikebu humwomba Allaah hali ya kumtakasia Yeye dini, lakini anapowaokoa katika nchikavu, tahamaki hao wanamshirikisha." (29:65)**

Walikuwa wakikubali kuwa Allaah pekee ndiye muumba. Amesema (Subhaanah):

وَلَئِن سَأَلْتَهُم مَّنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ

**"Ukiwauliza: "Ni nani aliyeumba mbingu na ardhi?" Basi watasema: "Allaah." (31:25)**

قُلْ مَن يَرْزُقُكُم مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ أَمَّن يَمْلِكُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَارَ وَمَن يُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَيِّتِ وَيُخْرِجُ الْمَيِّتَ مِنَ الْحَيِّ وَمَن يُدَبِّرُ
الْأَمْرَ ۚ فَسَيَقُولُونَ اللَّهُ ۚ فَقُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ

**"Sema: "Nani anayekuruzukuni kutoka mbinguni na ardhini au nani anayemiliki kusikia na kuona na nani anayemtoa aliye hai kutoka maiti na anayemtoa maiti kutoka aliye uhai na nani anayeendesha mambo yote? Watasema: "Ni Allaah", basi sema: "Basi kwa nini hamchi?" (10:31)**

Aayah zilizo na maana kama hii ni nyingi.

## 15. Washirikina wa leo ni waovu zaidi kuliko wale wa kale

Washirikina waliokuja nyuma wamewashinda wale washirikina wa kale kwa njia mbili:

**Ya kwanza:** Baadhi yao wameshirikisha katika uola wa Allaah.

**Ya pili:** Wanashirikisha katika kipindi cha raha na shida.

Hayo yanatambulika na wale waliochanganyika nao, wakazisoma hali zao na wakaona yale wanayoyafanya kwenye kaburi la al-Husayn, al-Badawiy na wengineo waliyoko huko Misri, kwenye kaburi la al-´Aydaruus huko Aden, al-Haadiy huko Yemen, Ibn ´Arabiy huko Shaam, Shaykh ´Abdul-Qaadir al-Jaylaaniy huko ´Iraaq na makaburi mengine yanayojulikana ambayo wajinga wameyapindukia mpaka kwa kuyafanyia mengi ambayo ni haki ya Allaah (´Azza wa Jall). Watu hawa wanatakiwa kukaripiwa na kubainishiwa Tawhiyd ya hakika ambayo Allaah amemtuma nayo Mtume Wake (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) na Mitume waliokuwa kabla yake (´alayhim-us-Swalaatu was-Sallaam). Tunamuomba Allaah awarudishe katika werevu wao, afanye kuwepo kati yao walinganizi wengi wa uongofu na awawafikishe wanachuoni wa waislamu waweze kupambana na shirki hii na waitokomeze na vilevile watokomeze njia zake. Hakika Yeye ni Mwenye kusikia na yukaribu.

## 16. Radd kwa Mu´tazilah, Jahmiyyah na Ashaa´irah

Miongoni mwa I´tiqaad vilevile zinazopingana na ´Aqiydah sahihi katika mlango wa majina na sifa za Allaah ni zile I´tiqaad za Ahl-ul-Bid´ah katika Jahmiyyah, Mu´tazilah na wale wenye kupita mapito yao katika kupinga sifa za Allaah (´Azza wa Jall) na kumkanushia (Subhaanah) kuwa na sifa kamilifu na wakati huo huo wanamsifu Allaah (´Azza wa Jall) kwa sifa zisizokuwepo, vitu visivyokuwa na uhai na ambavyo ni muhali - Allaah ametakasika kutokamana na maneno yao kutakasika kuliko kukubwa!

Wanaingia humo wale wenye kukanusha baadhi ya sifa na badala yake wakathibitisha baadhi yake tu. Mfano wa waliofanya hivo ni Ashaa´irah. Katika zile sifa walizothibitisha yanawalazimu yale yale waliyoyakimbia katika zile sifa walizokanusha na wakazifasiri kimakosa. Kwa hivyo wakawa wameenda kinyume na dalili za Qur-aan na Sunnah na za kiakili. Isitoshe wamejigonga kujigonga kuliko wazi kabisa.

Kuhusu Ahl-us-Sunnah wal-Jamaa´ah wamemthibitishia Allaah (Subhaahah) yale majina na sifa alizojithibitishia Mwenyewe au alizothibitishiwa na Mtume Wake Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kwa njia kamilifu. Sambamba na hilo wamemtakasa kutokamana na kufanana na viumbe Vyake. Ni matakaso yaliyo mbali na uchafu wa ukanushaji. Kwa hiyo wakawa wamezitendea kazi dalili zote na hawakupotosha wala hawakukanusha na wakasalimika na kujigonga kama walivyojigonga wengine. Tumetangulia kutaja hilo. Hii ndio njia ya uokozi na furaha duniani na Aakhirah. Vilevile ndio njia iliyonyooka waliyopita Salaf wa Ummah huu na maimamu wake. Hakika mwisho wa Ummah huu hautofaulu isipokuwa kwa yale yaliyowafanya wa mwanzo wao kufaulu. Nacho si kingine ni Kitabu na Sunnah na kuacha vile vyote vyenye kwenda kinyume navyo.

## 17. Uwajibu wa kumuabudu Allaah peke yake

Hakika wajibu na faradhi ilio kubwa kwa ambaye ´ibaadah ni yenye kumuwajibikia ni yeye kumuabudu Mola Wake (Subhaanah), Mola ambaye ndiye muumba wa mbingu na ardhi na ´Arshi kubwa aliyesema katika Kitabu Chake kitukufu:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ اسْتَوَىٰ عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يَطْلُبُهُ حَثِيثًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ وَالنُّجُومَ
مُسَخَّرَاتٍ بِأَمْرِهِ ۗ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ وَالْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

**"Hakika Mola wenu ni Allaah ambaye ameumba mbingu na ardhi katika siku sita kisha akalingana juu ya ´Arshi. Anafunika usiku kwa mchana, unaufuatia upesi upesi na jua na mwezi na nyota vyote vimetiishwa kwa amri Yake. Tanabahi! Ni Vyake Pekee uumbaji na amri. Amebarikika Allaah, Mola wa walimwengu." (07:54)**

Vilevile ameeleza (Subhaanah) sehemu nyingine katika Kitabu Chake ya kwamba amewaumba majini na wanaadamu ili wamuabudu. Amesema (Ta´ala):

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ

**"Sikuumba majini na wanaadamu isipokuwa waniabudu." (51:56)**

´Ibaadah hii ambayo Allaah kawaumba majini na wanaadamu kwa ajili yake ni kumpwekesha Yeye katika aina zote za ´ibaadah kama swalah, swawm, zakaah, hajj, rukuu, sujuud, kutufu, kuchinja, kuweka nadhiri, kuwa na khofu, kutaraji, kutaka uokozi, kutaka msaada, kutaka kinga na aina nyenginezo za du´aa. Katika hayo kunaingia vilevile kumtii (Subhaanah) katika yale yote aliyoamrisha na kuacha makatazo Yake kutokamana na vile Qur-aan na Sunnah vilivyofahamisha. Allaah (Subhaanah) amewaamrisha majini na watu wote ´ibaadah hii waliyoumbwa kwayo na akawatuma Mitume wote na akateremsha Vitabu kwa ajili ya kubainisha ´ibaadah hii, kuipambanua, kulingania kwayo na kuamrisha kumtakasia ´ibaadah Allaah peke yake. Amesema (Ta´ala):

يَا أَيُّهَا النَّاسُ اعْبُدُوا رَبَّكُمُ الَّذِي خَلَقَكُمْ وَالَّذِينَ مِن قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ

**"Enyi watu! Mwabuduni Mola wenu Ambae amekuumbeni na wale wa kabla yenu mpate kucha." (02:21-22)**

وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ

**"Mola wako ameamrisha, kwamba asiabudiwe yeyote isipokuwa Yeye pekee." (17:23)**

Maana ya "amehukumu" katika Aayah hii ni ameamrisha na ameusia. Amesema (Ta´ala):

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ ۚ وَذَٰلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

**"Hawakuamrishwa jengine isipokuwa wamuabudu Allaah kwa imani safi kabisa na ya asli hali ya kumtakasia Yeye dini, wasimamishe swalah na watoe zakaah - na hiyo ndiyo dini iliyosimama imara." (98:05)**

Aayah zilizo na maana kama hii katika Qur-aan ni nyingi. Amesema (´Azza wa Jall):

وَمَا آتَاكُمُ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانتَهُوا ۚ وَاتَّقُوا اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ

**"Yale alokupeni Mtume, basi yachukueni, na yale alokukatazeni, yaacheni. Na mcheni Allaah. Hakika Allaah ni mkali wa kuadhibu." (59:07)**

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

**"Enyi mlioamini! Mtiini Allaah na mtiini Mtume na wale wenye madaraka katika nyinyi. Mkizozana katika jambo lirudisheni kwa Allaah na Mtume mkiwa kweli mnamwamini Allaah na siku ya Mwisho. Hivyo ni njia bora na matokeo mazuri zaidi." (04:59)**

مَّن يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ

**"Atakayemtii Mtume, basi amemtii Allaah." (04:80)**

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَّسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ

**"Hakika tulituma katika kila ummah Mtume [awaamrishe watu wake] kwamba: "Mwabuduni Allaah na jiepusheni na twaaghuut [miungu ya uongo]."" (16:36)**

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ

**"Hatukutuma kabla yako Mtume yeyote isipokuwa Tulimfunulia Wahy ya kwamba: "Hakika hapana mungu wa haki isipokuwa Mimi - basi niabuduni!"" (21:25)**

الر ۚ كِتَابٌ أُحْكِمَتْ آيَاتُهُ ثُمَّ فُصِّلَتْ مِن لَّدُنْ حَكِيمٍ خَبِيرٍ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا اللَّهَ ۚ إِنَّنِي لَكُم مِّنْهُ نَذِيرٌ وَبَشِيرٌ

**"Alif Laam Miym. Hichi ni Kitabu ambacho Aayah Zake zimetimizwa barabara kisha zikapambanuliwa vizuri kutoka kwa Mwenye hikmah, Mjuzi wa yote; ili msiabudu yeyote isipokuwa Allaah. Hakika mimi ni muonyaji kwenu na mbashiriaji." (11:01-02)**

Hizi ni Aayah ambazo ziko wazi kabisa. Kuna Aayah nyenginezo katika Qur-aan zilizo na maana kama hiyo ambazo zote zinafahamisha juu ya uwajibu wa kumtakasia ´ibaadah Allaah peke yake na kwamba huo ndio msingi wa dini na mila. Vilevile zinafahamisha kuwa hiyo ndio hekima ya kuumbwa majini na watu, kutumwa Mitume na kuteremshwa Vitabu.

Kwa hiyo ni wajibu kwa wale wote ambao ´ibaadah ni yenye kuwawajibikia kulitilia umuhimu jambo hili na kulielewa na kutahadhari na yale waliyotumbukia wengi wenye kujinasibisha na Uislamu katika kupetuka mipaka kwa Mitume, waja wema, kujenga juu ya makaburi yao, kufanya makaburi yao ni mahali pa kuswalia, kuyajengea makuba, kuwaomba, kuwataka uokozi, kuwategemea, kuwaomba watatue haja na matatizo, kuwaponya wagonjwa, wawanusuru dhidi ya maadui na aina nyenginezo katika shirki kubwa. Imesihi kutoka kwa Mtume wa Allaah (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) yenye kuafikiana na yale yenye kufahamishwa na Qur-aan. al-Bukhaariy na Muslim wamepokea ya kwamba Mu´aadh (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) alisema kumwambia:

*"Je, unajua Allaah ana haki ipi juu ya waja na waja wana haki ipi kwa Allaah?" Mu´aadh akasema: "Allaah na Mtume Wake ndio wanajua zaidi." Ndipo Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) akasema: "Haki ya Allaah juu ya waja wamuabudu na wala*

*wasimshirikishe Yeye na chochote. Haki ya waja kwa Allaah asimuabudu yule asiyemshirikisha Yeye na chochote."*[8]

Kumepokelewa katika "as-Swahiyh" ya al-Bukhaariy ya kwamba Ibn Mas´uud (Radhiya Allaahu ´anh) amesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

*"Atayekufa hali ya kuwa anamuomba mwenza na Allaah, ataingia Motoni."*[9]

Muslim amepokea katika "as-Swahiyh" yake kupitia kwa Jaabir (Radhiya Allaahu ´anh) aliyesimulia kuwa Mtume (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) amesema:

*"Atayekutana na Allaah hali ya kuwa hamshirikishi Yeye na chochote ataingia Peponi, na atayekutana na Allaah hali ya kuwa anamshirikisha Yeye na chochote ataingia Motoni."*[10]

Kuna Hadiyth nyingi zenye maana kama hii. Haya ndio masuala muhimu na makubwa zaidi.

[8] al-Bukhaariy (5912), Muslim (30), at-Tirmidhiy (2643), Ibn Maajah (4296) na Ahmad (05/238).

[9] al-Bukhaariy (4227), Muslim (92) na Ahmad (01/374).

[10] al-Bukhaariy (129), Muslim (32) na Ahmad (03/157).

## 18. Hitimisho

Allaah amemtuma Muhammad (Swalla Allaahu ´alayhi wa sallam) kulingania katika Tawhiyd na kukataza shirki. Akafikisha (´alayhis-Swalaatu was-Salaam) yale Allaah aliyomtuma kwa njia nzuri kabisa. Aliudhiwa kwa ajili ya Allaah kwa maudhi makubwa. Pamoja na hivyo akayavumilia yeye pamoja na Maswahabah wake (Radhiya Allaahu ´anhum) katika kufikisha dini ya Allaah mpaka Allaah akaondosha katika kisiwa cha kiarabu masanamu na mizimu yote na watu wakaingia katika dini ya Allaah makundi kwa makundi. Wakayavunja masanamu yaliyokuwa pembezoni na ndani ya Ka´bah na al-Laat, al-´Uzzaa, Manaat na masanamu mengine yote yaliyokuwa katika makabila ya waarabu yakaangamizwa na kuvunjwa. Vilevile ikaangamizwa mizimu waliokuwa nayo. Neno la Allaah likanyanyuliwa na Uislamu ukadhihiri katika kisiwa cha kiarabu. Hapo sasa ndipo waislamu wakaelekea kulingania katika dini ya Allaah na kupigana Jihaad nje ya kisiwa cha kiarabu na Allaah akawaongoza kupitia wao wale waja waliotanguliwa na furaha na vilevile Allaah akaeneza haki na uadilifu kupitia wao katika sehemu kubwa ya ulimwengu. Kwa hayo wakawa ni maimamu wa uongofu na viongozi wa haki na walinganizi wa uadilifu na kutengeneza. Taabi´uun na waliowafuata kwa wema wakapita juu ya mfumo wao. Wakawa ni maimamu wa uongofu na walinganizi wa haki wenye kueneza dini ya Allaah. Wanawalingania watu katika kumuabudu Allaah peke yake na wanapambana katika njia ya Allaah. Wanafanya hivo kwa nafsi na mali zao. Hawajali kwa ajili ya Allaah lawama za wenye kulaumu. Basi Allaah akawapa nguvu, akawanusuru, akawapa ushindi juu ya wengine na akawatimizia yale Allaah aliyowaahidi katika maneno Yake (Subhaanah):

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

**"Enyi mloamini! Mkimnusuru Allaah Naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu." (47:07)**

وَلَيَنصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ الَّذِينَ إِن مَّكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنكَرِ ۗ وَلِلَّهِ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ

**"Bila shaka Allaah atamnusuru yule mwenye kumnusuru. Hakika Allaah ni Mwenye nguvu kabisa, Mwenye enzi. Ambao Tukiwamakinisha katika**

**ardhi, husimamisha swalah na hutoa zakaah na huamrisha mema na hukataza maovu. Kwa Allaah pekee ndio hatima ya mambo yote." (22:40-41)**

Baada ya hapo watu wakabadilika, wakafarikiana, wakachukulia usahali suala la Jihaad, wakaipa kipaumbele raha, wakafuata matamanio na kukadhihiri kwao maovu. Waliosalimika ni wale tu waliokingwa na Allaah (Subhaanah). Allaah akawabadilikia na akawatawalishia maadui wao. Hayo ni malipo ya yale waliyoyachuma. Hakika Mola Wako si mwenye kumdhulumu mja. Amesema (Ta´ala):

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ لَمْ يَكُ مُغَيِّرًا نِّعْمَةً أَنْعَمَهَا عَلَىٰ قَوْمٍ حَتَّىٰ يُغَيِّرُوا مَا بِأَنفُسِهِمْ

**"Hayo ni kwa kuwa Allaah hakuwa Mwenye kubadilisha neema yoyote Aliyoineemesha kwa watu mpaka wao wabadilishe yaliyomo ndani ya nafsi zao." (08:53)**

Ni wajibu kwa waislamu wote - serikali na wananchi - warejee kwa Allaah (Subhaanah), wamtakasie ´ibaadah Yeye pekee, watubie Kwake kwa yale yaliyopita katika mapungufu na madhambi yao. Vilevile wanatakiwa wakimbilie zile faradhi Allaah alizowawajibishia na wajiepushe na yale aliyowaharamishia. Wausiane na wasaidiane hayo.

Katika yaliyo muhimu kuliko hayo ni kusimamisha adhabu za Kishari´ah, kuwahukumu watu kwa Shari´ah katika kila kitu na kuhukumiwa kwayo. Sambamba na hilo kanuni zilizotungwa ambazo zinapingana na Shari´ah ya Allaah zinatakiwa kutokomezwa na watu wasihukumiane nazo. Badala yake inatakiwa kuwalazimisha wananchi wote hukumu ya Shari´ah.

Ni wajibu kwa wanachuoni kuwafundisha watu dini yao, kueneza mawaidha ya Kiislamu kati yao, kuusiana katika haki na kuwa na subira juu yake. Vilevile inatakiwa kuamrishana mema na kukatazana maovu na kuwashaji´isha viongozi katika hayo.

Ni wajibu kupiga vita ujamaa, Ba´thiyyah, kuwa na kasumba juu ya mataifa na misingi mingine yenye kuangamiza na madhehebu yanayopingana na Shari´ah. Kwa hayo Allaah atawatengenezea waislamu yale yaliyoharibika na kuwazuilia yale yenye maovu na vilevile atawarudishia utukufu wao uliotangulia na kuwanusuru dhidi ya maadui wao na atawamakinisha katika ardhi. Amesema (Ta´ala):

وَكَانَ حَقًّا عَلَيْنَا نَصْرُ الْمُؤْمِنِينَ

**"Ni haki daima Kwetu kuwanusuru waumini." (30:47)**

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

**"Allaah amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema kwamba: Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwa kabla yao, atawamakinishia dini yao aliyowaridhia, atawabadilishia amani badala ya khofu yao [kwa sharti] wananiabudu Mimi pekee wasinishirikishi na chochote. Na yeyote yule atakayekufuru baada ya hapo, basi hao ndio mafasiki." (24:55)**

إِنَّا لَنَنصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ

**"Hakika Sisi tutawanusuru Mitume Wetu na wale walioamini katika uhai wa dunia na siku watakayosimama mashahidi." (40:51)**

يَوْمَ لَا يَنفَعُ الظَّالِمِينَ مَعْذِرَتُهُمْ ۖ وَلَهُمُ اللَّعْنَةُ وَلَهُمْ سُوءُ الدَّارِ

**"Siku hazitowafaa madhalimu udhuru wao na watapata laana na watapata makazi mabaya." (40:52)**

Allaah (Subhaanah) ndiye mwenye jukumu la kuwatengeneza viongozi wa waislamu na manaibu wao, kuwatunuku uelewa katika dini, kuukusanya umoja wao juu ya uchaji Allaah, kuwahidi wote katika njia Yake iliyonyooka, kuinusuru haki kupitia wao, kuikosesha batili nusura kupitia wao, awaongoze wote kuweza kushirikiana katika wema na uchaji Allaah, kuusiana katika haki na kuwa na subira juu yake. Hakika Yeye ndiye muweza wa hayo.

Swalah na salaam zimwendee mja, Mtume Wake na kiumbe bora, Mtume wetu, kiongozi wetu na bwana wetu Muhammad bin ´Abdillaah, kizazi chake, Maswahabah wake na wenye kufuata uongofu wake.